



# Safari ya Amina



Tusome Early Literacy Programme

## Safari ya Amina



Amina aliamua kumtembelea shangazi yake.  
Aliamka asubuhi na kuanza kujitayarisha.  
Amina alitamani sana kucheza na binamu zake.

Jua lilikuwa kali sana.

Amina alihisi joto mwilini.

Mama yake alimwambia kuwa mvua  
ingenyesha baadaye mchana.





Amina alipuuza mama yake na kutoka nyumbani bila sweta.

Mama alimsindikiza Amina hadi kituo cha basi.

Hali ya hewa ilibadilika, kukawa na upepo.

Amina alihisi baridi.

Amina alikimbia nyumbani kuchukua sweta.

Alimkuta mama yake akiota moto.





Mama yake alimpa koti.

Pia, alimpatia mwavuli wa kujikinga mvua.

Amina alielekea tena kwenye kituo cha basi.

Amina alipanda basi kuelekea jijini.

Akiwa njiani, aliona gari la moshi lililokuwa limebeba mizigo mizito.

Vilevile, aliona dau ziwani likiwa na wavuvi.





Jijini, mvua ilikuwa inanyesha rasharasha.

Amina alipanda pikipiki ili afike kwa shangazi yake haraka.

Alipofika kwa shangazi, alipewa chai moto.



Baada ya muda mfupi, mvua iliisha.  
Hewa ilikuwa tulivu na jua likachomoza.  
Amina na binamu zake walienda uwanjani kucheza.

## Maswali

1. Amina aliamua kumtembelea nani?
2. Kwa nini Amina alihisi joto?
3. Kwa nini Amina alirudi nyumbani kutoka kituo cha basi?
4. Amina alimkuta mama yake akifanya nini?
5. Kwa nini mama alimpa Amina mwavuli?

# Safari ya Amina

Amina anaamua kumtembelea shangazi yake. Akiwa safarini, hali ya hewa inabadilika. Amina atasaidikaje?



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE



**UKaid**  
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.